OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

SHULE YA SEKONDARI MWASAMBA,
S. L. P 47,
BUSEGA,
15/12/2021

Kumb.Na.Mwss/J1/vol1/19/6
Mwanafunzi……..
Shule ya msingi……
BUSEGA.

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWASAMBA WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021</u>

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.shule ya sekondari Mwasamba ipo umbali wa kilometa 39 Kaskazini Mashariki ya mji wa Nyashimo, Halmashauri ya Wilaya ya Busega.
Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

a) Sare ya shule hii ni

WAVULANA:-

i. Suruali mbili (2) za rangi ya ugoro (brown) zenye marinda mawili kila upande, mkunjo wa chini “turn up” upana wa inchi 10. Kitambaa cha suruali kiwe chenye ubora wa juu kisichopauka haraka.
ii. Shati mbili (2) nyeupe aina ya tetroni yenye mikono mifupi. Isiwe ya kubana mwili.
iii. Mkanda mweusi

WASICHANA:-

i. Sketi mbili (2) rangi ya ugoro (brown). Upana wa marinda ya sketi uwe inchi 2. Sketi iwe ndefu inayovuka magoti. Sketi zisizofuata vipimo hivyo hazikubaliki, kitambaa cha sketi kiwe chenye ubora wa juu kisichopauka.

ii. Shati / blauzi mbili (2) rangi nyeupe aina ya tetroni yenye mikono mifupi isiwe ya kubana mwili.

WAVULANA NA WASICHANA WOTE

i. Viatu vya ngozi vyenye kufunika miguu na visiwe na visigino virefu wala mapambo yoyote.viatu viwe vya kufunga na kamba.
ii. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili zisizo na mapambo .
iii. Sweta la rangi ya ugoro (brown)

B: KWA WANAOVAA HIJAB. Rangi ya Hijab ifanane na sare ya shule (nyeupe)

C: SARE YA MICHEZO

WAVULANA

i. Bukta yenye rangi ya bluu
ii. Tisheti yenye rangi ya zambarau
iii. Raba za michezo

WASICHANA

i. Bukta yenye rangi ya bluu yenye mpira (elastic) yakubana miguuni
ii. Sketi fupi yenye rangi ya bluu
iii. Tisheti yenye rangi ya zambarau
iv. Raba za michezo

D. VIFAA VYA USAFI

1. Mwanafunzi aandaliwr mfagio wa chelewa kwa ajiri ya usafi wa mazingira
2. Kwa ajili ya kudeki Madarasa na kumwagilia maua aandaliwe ndoo ya lita 10

E. VIFAA VYA DARASANI

1. Madaftari yasiyopungua 12
2. Kalamu za kutosha, tula, kamusi ya kiingereza

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……..

L. M. MAKENZI

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI MWASAMBA

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, Walimu / Wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kujifunza kwa bidii shuleni na nyumbani.
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za umma.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA 'KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya Kama vile uvutaji bangi, Cocaine, mirungi, kubeli n.k.
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa mjamzito / kupata mimba
(i) Kuoa au Kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. **KIAMBATISHO "B".**

(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai na mzazi / mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. **KIAMBATISHO "A".**

(c) Tafadhari soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

3.

KIAMBATISHO "A"

FOMU YA MKATABA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWASAMBA

ANUANI YAKO ……..

…….

…….

TAREHE ……

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MWASAMBA,
S. L. P 47,
BUSEGA.

SEHEMU "A" IJAZWE NA MWANAFUNZI.

Mimi ……. Ambaye ni Mvulana / Msichana niliyekuwa nasoma shule ya msingi …… Wilaya ya ……. Mkoa wa ……. Nakubali / sikubali kujiunga na shule ya sekondari Mwasamba

Wilaya ya Busega Mkoa wa Simiyu leo tarehe ……. Nitazingatia na kutii sheria za shule na za nchi hii, nitakuwa mwaminifu, mwenye bidii na juhudi katika masomo, kazi za nje na michezo.

JINA LANGU …… SAHIHI: …….

TAREHE: ……

SEHEMU "B" IJAZWE NA MZAZI / MLEZI.

Mimi …… Mzazi / Mlezi wa ……..... ninayeishi Kitongoji cha …… Kijiji cha …… Wilaya ya ……. Mkoa wa …….. nakubali/ sikubali mtoto wangu kujiunga na kusoma katika shule ya Sekondari Mwasamba kuanzia tarehe …….. hadi atakapohitimu kidato cha nne. Mtoto wangu nitampatia mahitaji yote yanayotakiwa shuleni. Nitahakikisha ninafuatilia kwa ukaribu sana mahudhurio, mwenendo na maendeleo yake shuleni. Hivyo sitasita kumwonya na kuchukua hatua za kisheria pale anapobainika kutenda kinyume na sheria, Kanuni na taratibu za shule.

JINA LANGU …….. SAHIHI: ……..

TAREHE: …….....

4.

KIAMBATISHO B
PRIME MINISTER OFFICE –REGIONAL ADMNISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MWASAMBA SECONDARY SCHOOL ,
S. L. P BOX 157,
BUSEGA.

APPLICATION FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by medical officer in respect of all for one entrant

Student's full name …….

Age ……. (year). Sex …….

Blood count (red and white) ……...

Stool examination ……...

Urine analysis ……. Gestation for girls …….

Syphilis test …….

TB Test …….

Eye Test ……

Ears ……

Splcon ……

Chest …….

Abdomen ……..

ADDITIONAL INFORMATION E.g. Physical defects or impairment infections, chronic or family disease ……..……

……..……

……..……

I certify that the above named student is fit / unfit to pursue studies as stated above

Signature …….

Designation …….

Station …….

Date …….

Note: Medical Officer

At a time of examination, please treat the individual for any ailment you noted